**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**CHUO CHA UALIMU ILONGA**
**S.L.P. 98, KILOSA**
**Barua pepe: ilongatc@gmail.com**
**ilongatc@moe.go.tz**
**Namba ya simu: +255755 536 679**

Tarehe: **30/06/2026**

Ndugu…………………………………………………………….

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA STASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA MSINGI MWAKA 2026/2027**

1. **UTANGULIZI:**

*Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na mafunzo ya stashahada ya Ualimu katika **CHUO CHA UALIMU ILONGA**. Hii ni bahati ya pekee kwako kuwa mmojawapo wa wanachuo watakaopatiwa mafunzo ya **stashahada** ya Ualimu ELIMU YA MSINGI MCHEPUO WA SANAA NA MICHEZO. **MUDA WA MAFUNZO DIPLOMA YA KAWAIDA NI MIAKA MIWILI NA DIPLOMA KWA NJIA YA MASAFA NI MIAKA 3 HADI 4.***

**DIRA YA CHUO: Kuwa chuo kinachoongoza kitaifa katika kuandaa walimu bora na mahiri kwa manufaa ya Taifa**.

**DHAMIRA YA CHUO: Kuandaa mazingira mazuri ya kujifunza na kufundishia, kuendeleza walimu kitaaluma na kitaalamu kwa kutumia sayansi na Teknolojia, pia kuhifadhi tunu za Taifa.**

**MOTO WA CHUO:**"Elimu ni Uwezo".(Education is Power)

**MAHALI CHUO KILIPO.**

Chuo cha Ualimu Ilonga kipo mkoani Morogoro, wilaya ya Kilosa umbali wa kilometa 9 kaskazini mwa mji wa Kilosa.

Maeneo ya kupandia basi kwa wale wanaotokea barabara ya Dodoma, Singida, Mwanza, Tabora, Shinyanga n.k, kituo ni **Dumila** Kilosa. Kwa wale wanaotoka Dar es salaam, Tanga, Iringa, Moshi, Arusha n.k, na Watashuka morogoro mjini watapanda mabasi **Msamvu AU Mafiga-Morogoro**. Kituo utakachoteremkia ili kuelekea chuoni ni **Ilonga Msalabani** umbali wa kilometa moja toka hapo. Unaweza kutembea kwa miguu au kupanda pikipiki(Bodaboda), kwa kiasi kisichozidi **Tsh 1500/-**. Endapo utatokea Kilosa mjini, utalipa kiasi kisichozidi **Tsh 5000/=** kwa bodaboda, ikiwa utapanda gari nauli haitazidi **Tsh 3000/=**

Pia kwa watakaopanda **SGR kituo ni KILOSA** utazikuta bodaboda kuja chuo nauli **haizidi Tsh 5000/-**

## 2.0. MAHITAJI YA USAJILI KWA WANACHUO WOTE KAWAIDA NA MASAFA

### 2.1 Vyeti Na Vitambulisho

Ili uweze **kusajiliwa** Chuoni, utatakiwa uje na **vyeti halisi** vifuatavyo:-

i. **Cheti halisi** cha matokeo ya mtihani cha Elimu ya sekondari (KIDATO CHA SITA) kilichotolewa na Baraza la mitihani la Tanzania (ACSEE)
ii. **Hati ya matokeo**(Result slip) kwa waliomaliza kidato cha sita kabla ya cheti halisi kutoka.
iii. **Cheti halisi cha Kidato cha NNE (CSEE).**
iv. **Cheti cha astashahada kwa wale waliosoma daraja la IIIA.**
**v.** **Cheti halisi cha kuzaliwa**

## DIPLOMA YA KAWAIDA:

### 2.2 Ada:

Ada ya chuo ni **Tsh 450,000/=** kwa mwaka. **Malipo yote ya ADA wasiliana 0785786165, 0784975131,0762044614,0763594607** Ili upatiwe **CONTROL NUMBER** ya kulipia fedha hizo za Ada.

### 2.3 Michango

Kila mwanachuo, WA MIAKA MIWILI atatakiwa kuchangia michango kama ifuatavyo :

| MCHANGO | JUMLA KWA MWAKA | |
|---|---|---|
| Usajili na kitambulisho | 20,000 | **Kwa mwaka** |
| Ukarabati | 25,000 | Kwa mwaka |
| Serikali ya wanachuo | 5,000 | Kwa mwaka |
| Usafi, mazingira | 20,000 | Kwa mwaka |
| Kukodisha Godoro | 10,000 | Kwa mwaka |
| Ulinzi | 30,000 | Kwa mwaka |
| Michezo | 30,000 | Kwa mwaka |
| Huduma ya kwanza | 10,000 | Kwa mwaka |
| **JUMLA** | **150,000** | |

## ELIMU MASAFA

**KWA WANACHUO WALIOOMBA KUSOMA KWA NJIA YA MASAFA (WALIMU KAZINI) MICHANGO NI TSH 150,000/-** Fedha hii pia iingizwe kwenye akaunti ya michango. Ada ni 450,000, **Zingatia maelekezo ya utumaji wa fedha za ADA na Pia fedha za Michango.**

Fedha yote ya **MICHANGO YA KAWAIDA na MASAFA** ilipwe kwenye akaunti ya **NMB**, namba **21803100001** Jina la akaunti ni **Local Ilonga Teachers' College**. Tafadhali **andika jina la mwanachuo anayelipiwa/anayelipa**. **Malipo yote ya ADA wasiliana 0785786165, 0784975131,0762044614,0763594607** Ili upatiwe **CONTROL NUMBER** ya kulipia fedha hizo za Ada.

**NB: -Tafadhali usichanganye fedha ya Ada na michango kwenye akaunti moja. Soma maelekezo yaliyotolewa hapo mwanzo ya namna ya kulipia ADA**

- Uje na nakala za malipo ya benki (pay in slips) kuthibitisha malipo. Unaweza kulipa nusu kwa kila muhula.

## 3.0 SARE YA CHUO KWA WANACHUO WA KAWAIDA

**Kila mwanachuo anatakiwa KUJA na sare kama ifuatavyo.**

**(i ) WANAWAKE:**

- Mashati mawili mikono mirefu-**Light Blue**
- Sketi nyeusi mbili za heshima (**urefu unaopita magoti kwenda chini** ) Mshono wa moja kwa moja wenye mpasuo wa kufunika nyuma (overlaping), kitambaa kiwe cha suti ya kiume kisicho na mng'ao wala mistari,
- Viatu vyeusi vyenye visigino vifupi,
- **Tai nyeusi, Koti jeusi, Soksi nyeusi,**
- Kwa wanachuo Waislam watavaa suruali nyeusi, nusu kanzu (panjab) ya rangi ya bluu bahari na **juba nyeusi inayoishia kwenye vitanga vya mikono**,
- T-Shirt yenye nembo ya chuo ni lazima uwe nayo inapatikana Chuoni. Uje na Tsh. 20,000/= .

**(ii) WANAUME:**

- Mashati mawili mikono mirefu – **Light Blue,**
- Suruali mbili nyeusi zenye malinda mawili kila upande wa mbele mfuko mmoja nyuma,
- Viatu vyeusi vya kufunika miguu,
- **Tai nyeusi pana na ndefu, Koti jeusi, Soksi nyeusi ,**
- T-Shirt yenye nembo ya chuo ni lazima uwe nayo inapatikana Chuoni. Uje na Tsh. 20,000/= .

**PIA** Wanachuo wa kiislamu waje na nguo maalumu kanzu kwa wavulana na baibui nyeusi kwa wasichana kwa ajili ya matumizi ya **siku ya Ijumaa/skukuu** watokapo nje ya chuo kwenda kwenye ibada ya Ijumaa na skukuu.

### 3:9 Sare za Michezo

**KWA KUWA HIKI NI CHUO CHA MICHEZO**, Njoo na Track-suit ya rangi '**Dark blue'**(ADIDAS) T-shirt ( **jezi ya bluu isiyo na nembo/jina**), (kwa wavulana na wasichana). **Siku ya kuripoti vaa full track-suit na raba nyeupe za michezo.**

Bukta mbili rangi ya bluu (adidas), viatu vya mpira wa miguu ( njumu ikiwezekana) – wavulana, skintight 2 rangi nyeusi (ndefu), stocking za rangi ya bluu, raba nyeupe za kamba, sketi maalumu za michezo kwa wasichana ,filimbi/stopwatch ni **lazima uje na vifaahivyo**

### 4.0. MAHITAJI YAKO MUHIMU

Uje na vitu vifuatavyo ;- shuka mbili nyeupe, foronya mbili nyeupe, shuka mbili rangi bluu kwa wanaume, pinki kwa wanawake zote zisiwe na maua, mto mmoja, na chandarua nyeupe kwa ajili ya kuzuia mbu, Ndoo za kufulia na kutunzia maji ya kunywa. Pia uje na (1) RIMU ya kuprintia, (2) hardbroom/softbroom na (3) Chelewa lenye mkono.

**5.0 MAHITAJI YA TAALUMA**

Uje na vitu vifuatavyo : daftari 10 (counter book quare 2) na Msomi 10, mathematical set, penseli HB, mafaili 03 (flat files), rula ya sm 30 na kalamu za kutosha. Vifaa hivi vinapatikana kwenye maduka yaliyopo jirani na Chuo. UJE NA 10,000/- YA MAHAFALI YA CHUO YA 2026/2027.

**6.0. AFYA**

Uje na fomu iliyojazwa na daktari wa wilaya au mkoa baada ya kuthibitishwa afya yako . Endapo una ugonjwa wa kudumu njoo na vyeti vya Daktari pamoja na dawa ambazo huwa unazitumia. Njoo na kadi ya **BIMA YA AFYA, AU NJOO NA TSH 50400 KWA AJILI YA KULIPIA BIMA YA AFYA.**

**7.0. MAHITAJI MENGINE**

Utatakiwa kuja na;-Vyombo vya kulia chakula kama vile sahani, kikombe, vijiko, umma n.k, galoni ya maji yenye ujazo wa lita (tano kwa ajili ya maji ya kunywa, ndoo ya ujazo wa lita (10) kumi au zaidi (vifaa hivi vinaweza kupatikana kwenye duka la Chuo), Uje na fedha za kutosha kwa matumizi yako binafsi. Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa namba **0784975131, 0784 705316,0787432590, 0652838127**

**8:0. Mwanachuo ambaye hatakamilisha maagizo yote HATASAJILIWA.**
**Siku ya kuripoti vaa full track-suit na raba nyeupe za michezo ili upokelewe**

**NB:** Utakapofika chuoni uje na fomu hii.

I. Unatakiwa kuripoti chuoni kuanzia tarehe **17.08.2026** mwisho wa kuripoti ni tarehe **30.08.2025** baada ya hapo hutapokelewa chuoni.

**II. Nguo za nyumbani zinahitajika chache sana**


**MAJID SHITAMBALA MWALYEGO**
**MKUU WA CHUO**

Mkuu wa Chuo
Chuo cha Ualimu Ilonga
KILOSA

**NAKALA,**

**KATIBU MKUU,**
**WIZARA YA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA,**
**S L P 10, DODOMA.**

# SARE YA CHUO



APPENDIX 'A'
GOVERNMENT OF TANZANIA
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

FORM NO.I

PART A:

TO THE MEDICAL OFFICER ……………………………………………… ……………………………………………… ………………………………………………

FROM ILONGA TEACHERS' COLLEGE BOX 98,KILOSA

Name of examinee ………………………………………………………………………………

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full – time student. The Examination should include the following category ( i- iii).Each category or sub- category of which will ender the applicant ineligible in case of defect. Pregnancy (category iv) will also render a girl student ineligible for student.

1 (a)Eye – sight
(b)Hearing
©Speech
(d)Limbs
3.Neuroses
4.Other serious diseases
5.Pregnancy

DATE

PRINCIPLE
ILONGA TTC

PART: B

MEDICAL CERTIFICATE
(TO BE COMPLETTED BY GOVERNMENT MEDICAL OFFICER)

I have examined the above named and considered that he/she is physically fit a full time student

1 (a)Eye – sight …………….
(b)Hearing …………………..
© Speech …………………..
(d) Limbs ……………………..
(e)Venereal diseases …………………
(f)Leprosy ……………………
(g)Epilepsy ………………..

2. Neuroses……………………………………………………………
3. Other serious diseases…………………………………………………
4. Pregnancy ………………………………………………………………

Station …………………………………… Designation ………………………………

6 | P a g e